Mkombozi Centre for Street Children

Idara ya Elimu

JARIDA

Taarifa ya Robo Mwaka
(Julai - Septemba 2005)

Matokeo muhimu kwenye Sensa ya Mkombozi ya mwaka 2005

Uandikishaji wa shule kwa wavulana ni 85.9% na wasichana ni 80.5% mkoani Kilimanjaro. Na Arusha inashtua kwani uandikishaji kwa wavulana ni 57.6% na wasichana ni 79.63%. Licha ya jitihada nyingi zilizofanywa chini Mpango wa Maendeleo kwa Elimu ya Msingi ili kufikia Elimu ya Msingi Kwa Wote matokeo haya yanaonyesha jitihada za ziada zinahitajika kufanywa na mamlaka ili kuhakisha watoto wanaandikishwa na kwenda shule. Licha ya mafanikio katika kufuta ada za shule katika miaka ya hivi karibuni idadi ya watoto wanoacha shule imeongezeka Moshi na Arusha, isipokuwa idadi ya watoto wa mitaani wa muda imepungua Moshi kutoka 51 mwaka 2003 hadi 22 mwaka 2005.

Utafiti kuhusu kufanya kazi na wasichana walio katika mazingira magumu

Katika mwezi Septemba, walimu wa Mkombozi walifanya utafiti kuona uwezekano wa kufanya kazi na wasichana wanaoishi katika mazingira magumu. Unyanyasi wa kimapenzi umeongezeka na kuna haja ya haraka kwa mkombozi kusaidia sehemu salama ya kuishi watoto wa kike na nafasi ya wao kuondokana na umalaya na maisha ya mitaani. Uchambuzi wa awali unaonyesha kwamba 78% ya watu waliohojiwa walidhani kwamba wasichana wanakosa elimu kama tatizo kubwa. 50% ya waliohojiwa walisema tatizo hili linasababishwa na wazazi kushindwa kuwaelimisha watoto wasichana. 38% waliamini kwamba wasichana wanaoacha shule wanaajiriwa kama wafanyakazi wa majumbani. 46% wanaamini kwamba kuna wasichana wengi walio katika mazingira magumu na 75% walisema hakuna asasi zinayofanya kazi na watoto wa kike. 71% walidhani kama kuna huduma ya kuwapa wasichana, ni elimu . Hata hivyo wasichana wa Majengo waliohojiwa wenyewe 68% walikuwa wamemaliza shule ya msingi. Kutokuwa na nafasi ya kuendelea na masomo baada ya shule ya msingi hasa kwenda kwa stadi za kazi kumewafanya kukimbilia mitaani, kuingia kwenye umalaya au ajira za majumbani.

Databesi kwa ajili ya kusimamia taarifa za watoto sasa iko tayari

Utengenezaji wa mwanzo wa databesi kwa ajili ya kusimamia taarifa za watoto ulimalizika katika robo hii ya mwaka. Databesi itawezesha Mkombozi kusimamia maendeleo ya kila mtoto wakati wote, zikiwemo huduma zilizopokelewa, na vilevile idadi ya watoto ambao wamehudumiwa. Ina taarifa mbalimbali, pamoja na nyanja zote za shughuli za Mkombozi kuanzia shughuli za kielimu, tathmini, huduma za afya, mawasiliano barabarani, mawasiliano katika maeneo tunayofanya nayo kazi, mipango tunayopanga na watoto, mpaka maendeleo ya kisaikolojia. Tarehe 1 Novemba 2005 walimu watapewa mafunzo kuwawezesha kuingiza taarifa za watoto ambao wako chini yao. Taarifa zitaingizwa kuanzia za nyuma hadi Aprili 2005.

Mifano dhahiri ya tafiti shirikishi

Mifano dhahiri iliyokusanywa na timu ya watafiti shirikishi inatoa maelezo kuhusu hali za watoto walio katika mazingira magumu na mipango ya kuwasaidia. Imeonekana kuwa katika kila kesi kuna uwezekano wa kamati ya shule, serikali ya kijiji na mwalimu mkuu kwa pamoja kutatua hali za watoto walio katika mazingira magumu. Kwa mfano:

Kijiji cha Mnini:

Anthony Mtupili* anaishi katika kijiji cha Mnini na watoto 8. Kati yao hakuna ambaye amewahi kuwa shule. Timu ya watafiti ya shule na Afisa Mtendaji wa Kijiji walipotembelea, Anthony Mtupili alieleza kuwa hana uwezo wa kuwapeleka watoto wake shule, na vile vile mabinti zake wawili ni waja wazito, wawili wanafanya kazi za ndani kwenye familia nyingine na wawili wengine wameacha shule ya chekechea. Timu ya watafiti na serikali ya kijiji cha Mnini itafanya kazi pamoja kuhakikisha baadhi ya watoto wa watoto wa Mafara (kama sio wote) wanaanza shule.

Shule ya msingi Manushi Juu:

Timu ya watafiti imegundua kuwa Kulwa Mani* mtoto wa darasa la tano kutoka shule ya msingi Manushi Juu alikuwa na tabia ya utoro uliokithiri. Pia iligundulika Kulwa anaishi na mama na baba wa kambo, na wakati mwingine na babu yake. Timu ya watafiti ilipotembelea iligundua Kulwa haendi shule kwa sababu wazazi wake walikuwa wakimshurutisha afanye kazi shambani wakati wa kwenda shule, na shamba liko mbali sana na nyumbani. Timu ya watafiti imesaidia na kuhakisha kuwa Kulwa anakwenda shule na wazazi hawampeleki shambani wakati wa kwenda shule.

***Kumbuka:** Jina limebadilishwa kwa ajili ya kutunza siri.

MEMKWA ya Mkombozi na MEMKWA ya Serikalini

MEMKWA ya Mkombozi inamlenga mtoto mwenyewe na mafunzo ya vitendo ili kutoa elimu ambayo inapelekea kujitegemea. MEMKWA ya serikali inatumia elimu ya awali ili kuongeza uandikishwaji watoto katika shule za msingi nchini Tanzania. Mitazamo hii miwili ni tofauti kabisa na inamatokeo fulani kwa elimu ya Tanzania na kwa watoto walio katika uangalizi wetu. Uzoefu wa Mkombozi unaonyesha elimu ya MEMKWA inayotolewa na serikali haikidhi mahitaji ya watoto wasio mashuleni (hasa wale walio na mahitaji maalum) na kuna upungufu ambao unahitaji kutatuliwa ili MEMKWA iweze kutoa huduma yake ipasavyo.

Mkombozi inapendelea elimu yenye mahusiano zaidi, yenye kuleta mabadiliko, na yenye kuangalia mbele.

Vituo vya MEMKWA vyachaguliwa kwa ajili ya mafunzo

Mkombozi inadhamiria kulinganisha mwaka hadi mwaka mwingine watoto ambao wameandikishwa katika kila kituo cha cha MEMKWA ili kufanya tathmini ya mahitaji ya kielimu na misaada inayotolewa kwa watoto. Kwa kuwa kuna vituo vingi vya MEMKWA nchini Tanzania, Mkombozi itachagua kwa umakini vituo vya MEMKWA ambavyo vinafanya kazi kwa kufuata taratibu zifuatazo:

- Kituo kiwe katika eneo ambalo Mkombozi inafanya nalo kazi;
- Kituo kiwe na mahusiano ya kikazi na shule kumi ambazo Mkombozi inafanya nazo kazi (kwa ajili bajeti) au katika kata ili mtoto ambaye anamaliza katika kituo cha MEMKWA aweze kuingizwa katika moja ya shule ambazo Mkombozi inafanya nazo kazi.

Mradi wa elimu umechagua vituo vifuatavyo vya MEMKWA kutokana na vigezo vyake:

- Mwenge, Mandela, Rau na Shaurimoyo katika Manispaa ya Moshi.
- Mwasikusini, Kombo, Kimanganuni na Manushi Juu katika wilaya ya Moshi Vijijini.
- Narumu and Elerai katika wilaya ya Hai.

Kusaidia watoto walio katika mazingira magumu ambao hawawezi kupata elimu

Mikutano ya jamii ilifanywa katika shule za msingi Kibaoni na Pasua na kikundi cha ngoma cha Mkombozi. Lengo lilikuwa ni kuamsha ufahamu juu ya umuhimu wa elimu na kujua mbinu zilizoko kwenye jamii za kusaidia watoto walio katika mazingira magumu ambao hawana uwezo wa kwenda shule. Matokeo muhimu katika utafiti huu yameonyesha kwamba kuna kutokuaminiana kwa kiwango fulani kati ya shule na wazazi hasa kwa wale wazazi wasiojiweza. Hii inalingana na matokeo utafiti shirikishi uliofanyika ambao unaonyesha:

- Wazazi kulaumiwa kwa utoro wa watoto ni kawaida mashuleni. Walimu wanasema visababishi vya nje ndio vinawafanya watoto kutoenda shule, mfano kuzuiwa na wazazi, ujinga wa wazazi, na wazazi kutothamini elimu.
- Palipo na watoto wengi walioacha shule, shule haionekani kama ni ya thamani kwa jamii husika. Shule ya Lambo inasema matatizo mengi ya shule husababishwa na kuzungukwa na ulevi. Katika jamii ya Rau watu wanazungumzia utumiaji wa bangi na umalaya katika jamii kama visababishi vya kuacha shule kwa watoto.
- Kuna ushirikiano mdogo kati ya walimu na wazazi. Kila kundi lilikuwa na mtazamo wa kugombana, walimu wakiwalaumu wazazi kwa watoto kutokwenda shule na wazazi wakidhani elimu inayotolewa na walimu haina thamani.
- Walimu na jamii inawalaumu watoto wenyewe kwa kutokwenda shule, wakisema kuiga tabia za wanarika wenzao, kutokua na nidhamu na uvivu husababisha utoro shuleni.

~ P.O. Box 9601 Moshi, Tanzania ~ Tel: (255) 27 2754793 ~ Fax: (255) 27 2753410 ~
~ info@mkombozi.org ~ http://www.mkombozi.org ~